Toleo Maalum

# jarida la WIZARA YA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO

Jarida la Mtandaoni | www.michezo.go.tz | Septemba 06, 2022



# Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo




# Tamasha la JAMAFEST Linasaidia Kukuza Ushirikiano wa Kikanda

Na Eleuteri Mangi - WUSM

Tanzania inashiriki Tamasha la Tano la Sanaa na Utamaduni la Jumuiya ya Afrika Mashariki (JAMAFEST) 2022 ambalo linafanyika nchini Bujumbura Burundi likiongozwa na Kaulimbiu "Kutumia Rasilimali za Kiutamaduni kukabiliana na Athari za UVIKO-19 kwa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki".

Akifungua tamasha hilo Septemba 5, 2022 katika Uwanja wa Intwari Bujumbura nchini humo, Rais wa Jamhuri ya Burundi Mhe. Evariste Ndayishimiye amewashukuru Wakuu wa nchi za jumuiya hiyo kufanikisha vikundi vya Utamaduni na Sanaa kushiriki Tamasha la JAMAFEST 2022 kwa mafanikio nchini Burundi.

"Tukio hili husaidia sio tu ubadilishanaji wa kisanii na kitamaduni, lakini pia hukuza ushirikiano wa kikanda. Kuweza kuandaa tamasha hili la Sanaa na Utamaduni nchini Burundi, ni dalili tosha kwamba UVIKO 19 ipo nyuma yetu ushahidi kwamba jumuiya yetu ni thabiti na kwa pamoja tunaweza kukabiliana na changamoto yoyote" amesema Rais Mhe. Ndayishimiye.

Awali akiwakaribisha washiriki wa tamasha hilo Rais Mhe. Ndayishimiye, amesema kutoka nchi mbalimbali za Jumuiya ya Afrika Mashariki amesema wafurahie sio tu hewa ya Burundi, bali watafurahia madhari nzuri ya Ziwa Tanganyika, kula samaki aina ya mgebuka,dagaa na kuhe ambao wanapatikana katika ziwa Tanganyika.

Aidha, Rais Mhe. Ndayishimiye amesisitiza umuhimu wa Tamasha hilo na kusema kuwa linanaongeza kuimarisha umoja na muingiliano kati ya watu wa wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Tamasha la JAMAFEST linafanyika kwa mzunguko ambapo mwaka 2022 ni zamu ya nchini Burundi baada ya kufanyika tamasha la 4 kufanyika kwa mafaniko makubwa jijini Dar es Salaam 2019.











# Msanii Mrisho Mpoto Anyanyua Shangwe JAMAFEST Nchini Burundi

Na Eleuteri Mangi - WUSM

Msanii maarufu katika kughani mashairi nchini Tanzania Mrisho Mpoto, maarufu 'Mjomba' amepeperusha vema bendera ya Tanzania Tamasha la Tano la Sanaa na Utamaduni la Jumuiya ya Afrika Mashariki (JAMAFEST) nchini Burundi.

Msanii Mjomba amekonga nyoyo za washiriki wa Tamasha la JAMAFEST na wananchi wa Burundi kwa wimbo wake wa "Wewe ni nani" wakiongozwa na Rais wa Jamhuri ya Burundi Mhe. Evariste Ndayishimiye ambaye alikuwa Mgeni Rasmi katika ufunguzi wa tamasha hilo.

Akishangiliwa na mamia ya watu waliohudhuria ufunguzi wa tamasha hilo Setemba 5, 2022 katika uwanja wa michezo wa Intwari Bujumbura, Mjomba amesisitiza wananchi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kutambua thamani ya utamaduni wao ambao ndiyo alama inayowapa heshima na kujitofautisha na mataifa mengine.

Katika ufunguzi huo, kila nchi mwanachama wa Jumuiya hiyo walikaribishwa kutoa ujumbe na kuburudisha hadhira, ndipo zamu ya Tanzania ilipofika ilikuwa shangwe na nderemo kumuona msanii Mpoto akiingia akiwa taika mavazi ya asili na kucheza kwa mtindo wa Kiafrika kwa kuonesha sarakasi safi, kutumia moto bila kuungua na kuuzima, kuonesha umahiri wa kuchezesha vifaa kwa kutumia miguu ikiwemo kuzungusha ngoma na kubeba meza.

Tamasha la JAMAFEST linafanyika kwa mzunguko ambapo mwaka 2022 ni zamu ya nchini Burundi baada ya kufanyika tamasha la 4 kufanyika kwa mafaniko makubwa jijini Dar es Salaam 2019.


RE FESTIVAL
OUTH SUDAN







# WIZARA YA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO

## Limeandaliwa na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini - GCU

**Mawasiliano**
P.O. Box 25, Dodoma,Tanzania
Mji wa Serikali Mtumba
Telephone: +255 26 2322 129
Nukushi: +255 26 2322 128
Barua pepe: km@habari.go.tz